


Research Article

Section: Literature, Linguistics & Criticism

Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global.

Volume 4, Issue 2, 2023

**Article Information**
Submitted: 18th October 2022
Accepted: 4th February 2023
Published: 21st March 2023

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

To read the paper online, please scan this QR code

**How to Cite:**
Muia, S. T., Mutua, J., & Makoti, V. (2023). Usawirishaji wa Uhusika katika riwaya za Rosa Mistika na Maisha Kitendawili. *Research Journal in African Languages*, 4(2). Retrieved from https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/1053

# Usawirishaji wa Uhusika katika riwaya za Rosa Mistika na *Maisha Kitendawili*

**Shadrack Tete Muia, John Mutua & Vifu Makoti**
Department of Linguistics and Languages, Machakos University, Kenya
Correspondence: shadracktete@gmail.com
https://orcid.org/0000-0003-2473-8539


**Abstract**
This article examines the nature of characterization in *Rosa Mistika* and *Maisha Kitendawili*. It contends that characterisation is very important aspect in literary work because it brings out the themes and various features of style in the texts. This literary elements relies on various aspects like style, structure, characters, scenery and use of language. The aspect of characters is very important in literary work because it involves all other aspects and discipline so as to give out the theme in literary work. Characters are created in a creative manner by the authors so that they can take different roles inorder to differentiate them and make the audience realize the traits of a certain character from another in literary work. The aim of this paper is to identify the similarities of the main characters and their character traits in the novels of *Rosa Mistika* (Euphrase Kezilahabi) and *Maisha Kitendawili* (John Habwe). This paper is guided by the theory of existentialism. This theory has made the researcher identify characters traits of the main characters as portrayed by the authors. Thus; this article examines the uniqueness of characterization in Rosa *Mistika* by Euphrase Kezilahabi and *Maisha Kitendawili* by John Habwe. This paper is guided by the theory of existentialism.

**Keywords:** character, characterisation, context, imagination, literary imagination, unique characterisation

© 2023 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

Research Journal in African Languages

RJAL




Research Article

Section: Literature, Linguistics & Criticism

Check for updates

Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global.

Volume 4, Issue 2, 2023

**Article Information**
Submitted: 18th October 2022
Accepted: 4th February 2023
Published: 21st March 2023

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

To read the paper online, please scan this QR code

**How to Cite:**
Muia, S. T., Mutua, J., & Makoti, V. (2023). Usawirishaji wa Uhusika katika riwaya za Rosa Mistika na Maisha Kitendawili. *Research Journal in African Languages*, 4(2). Retrieved from https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/1053

# Usawirishaji wa Uhusika katika riwaya za Rosa Mistika na *Maisha Kitendawili*

**Shadrack Tete Muia, John Mutua & Vifu Makoti**
Department of Linguistics and Languages, Machakos University, Kenya
Correspondence: shadracktete@gmail.com
https://orcid.org/0000-0003-2473-8539

**Ikisiri**
Makala hii inajadili usawirishaji wa uhusika katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili*. Kipengele cha wahusika ni muhimu katika kazi ya fasihi kwani hushirikiana na vipengele vingine vya fani ili kutoa ujumbe wa kazi ya fasihi. Kwa kawaida wahusika hujengwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwasilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii. Kwa hivyo lengo la makala hii ni kuchambua uwashirishaji wa wahusika wakuu katika riwaya za *Rosa Mistika* ya Euphrase Kezilahabi na *Maisha Kitendawili* ya John Habwe Kwa kawaida wahusika hujengwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwasilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii. Kipengele cha wahusika ni muhimu katika kazi ya fasihi kwani hushirikiana na vipengele vingine vya fani ili kutoa ujumbe wa kazi ya fasihi. Mwandishi huwajenga wahusika wake kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kuwatofautisha na kuiwezesha hadhira yake kutambua sifa za mhusika fulani na kutofautisha na mhusika mwingine katika kazi ya fasihi. Kwa hivyo lengo la makala hii ni kubainisha mfanano wa wahusika wakuu katika riwaya za *Rosa Mistika* (Euphrase Kezilahabi) na *Maisha Kitendawili* (John Habwe). Ili kufikia lengo la makala hii tumeongozwa na nadharia ya udhanaishi. Nadharia hii imetuwezesha kubainisha sifa za wahusika wakuu kama zilivyosawiriwa na waandishi.

**Maneno Muhimu:** fani, mbinu, mtindo, sanaa, uhusika, usawiri, wahusika

© 2023 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

**Public Interest Statement**
Characters are personages in a creative work of art while the nature of characterisation is the art of imagining and portraying characters in enough detail that they seem real both to the author and the audience. Thus, the nature of characterisation provides a human element that allows readers to imagine themselves inside the story. In order to be convincing, fictional characters must ring true. This forms the basis around which this paper analyses the nature of characterisation in Rosa *Mistika* by Euphrase Kezilahabi and *Maisha Kitendawili* by John Habwe.

**Utangulizi**
Fasihi hutegemea uwezo wa msanii wa kuzua au kubuni kutokana na yale yanayojitokeza katika jamii. Anapobuni kutokana na matukio katika jamii, hulazimika kuwaumba wahusika na kuwatumia kuyaeleza matukio hayo. Kimsingi wahusika huwa malighafi wanayoitumia waandishi wote wa kazi tofauti za fasihi. Sheria ndizo huongoza namna ambavyo waandishi hao watachota kutoka kwa malighafi hiyo na jinsi umbo la kazi ya fasihi wataibuka nayo. Wahusika pia huwa matokeo ya akili ya mwandishi, kwani ni viumbe wa akilini mwa mwandishi ambao huwekwa katika maandishi ili kutekeleza wajibu kulingana na lengo la mwandishi. Sifa za wahusika hufichua mitazamo ya msanii anayehusika kumhusu mhusika fulani.

Kazi mbalimbali za kifasihi huwa na sheria ambazo huongoza watunzi wa kazi hizo katika kuteua wahusika. Katika kuumba wahusika, mwandishi huchota mawazo, hulka, matendo pamoja na kauli zao kutokana na maisha ya jamii yake akiongozwa na lengo lake. Wahusika wa fasihi wanaweza kuwa viumbe wa kila aina kama binadamu, wanyama, ndege, mazimwi na hata vitu visivyo hai. Mara nyingi fasihi simulizi huhusishwa na wahusika changamano, yaani mwandishi anaweza kutumia wahusika binadamu, wanyama au vitu visivyo hai. Fasihi andishi hutumia wahusika binadamu. Hata hivyo, baadhi ya watunzi hutumia wahusika wanyama katika riwaya zao ili kujiepusha na shari itokanayo na kuwazungumzia baadhi ya watu wanaopatikana katika jamii ya mwandishi. Mfano wa mwandishi aliyewateua wahusika wanyama ni George Orwell katika riwaya ya *Shamba la Wanyama* (tafsiri ya 1967). Wahusika hawa hupewa sifa ambazo huwakilisha matendo yao katika kazi ya mwandishi.
Ujumbe wa mwandishi hufikia wasomaji kupitia kwa matendo na mazungumzo ya wahusika wake. Wahusika hutumika kuwasilishwa dhana mbalimbali katika jamii. Dhana hizi za wahusika hutumiwa kufurahisha, kuarifu na kuifahamisha msomaji kuhusu Jambo fulani. Kimsingi, kazi ya fasihi ni mkusanyiko wa matendo tofauti ya wahusika mbalimbali walio na nafasi katika kuendeleza hadithi fulani. Wahusika pia hutumiwa kuwasilisha fikra za mwandishi. Kwa kawaida, waandishi huumba watu wanaowafahamu na wakati mwingine wakajiumba wenyewe katika hadithi zao. Pia wahusika wa kazi za fasihi hutuwezesha kuwaelewa binadamu kuliko tunavyowaelewa watu tunaotangamana nao kila siku. Sababu hii huwezesha mwandishi kuonyesha maisha ya siri na mawazo ya ndani ya mhusika wake.

Mwandishi anaweza kuumba mhusika kwa kutumia njia mbalimbali ili kufikia lengo lake. Njia hizi ni pamoja na lugha na fikra ya wahusika, umbo la mhusika na matendo yao. Lugha anayoitumia mhusika inaweza kutumika kufafanua mengi kumhusu mhusika pamoja na uhusiano wake na wenzake. Umbo lake linaonyeshwa kutokana na yale yanayoonekana wazi kama umbo la mwili na mavazi anayoyavaa. Matendo hutumika kusawiri mhusika kulingana na uwezo na tabia zake katika hadithi. Matendo hayo hudhihirika wazi katika hadithi ya mwandishi. Licha ya riwaya hizi kuandikwa katika karne tofauti; *Rosa Mistika,* karne ya ishirini na *Maisha Kitendawili* karne ya ishirini na moja, waandishi Euphrase Kezilahabi na John Habwe wamewasawiri wahusika wakuu wenye sifa sawia. Katika makala hii tumeonyesha jinsi wahusika wakuu walivyo na sifa sawia na yaliyowakumba wahusika hao katika riwaya za waandishi hawa.

**Dhana ya udhanaishi**

Mwandishi wa makala hii anaongozwa na nadharia ya udhanaishi ili kushughulikia kipengele cha wahusika katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili*. Kulingana na Wamitila (2003) udhanaishi ni dhana inayotumiwa kuelezea falsafa ya kuwako na maisha. Wanjala Simiyu (2011) naye anasema udhanaishi ni mtazamo wa maisha ulio na kitovu chake katika swala kuwa, maisha ni nini na yana maana gani kwa binadamu? Ni kwa njia gani mwanadamu anaweza kuyabadilisha maisha yake yaliyojaa dhiki, mashaka na huzuni. Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007) udhanaishi hutilia mkazo matatizo halisi yanayomsibu mwanadamu na juhudi za mtu binafsi kupambana na maisha huishia katika ukengeushi au hukutwa na mauti. Udhanaishi unaelezea jinsi mwanadamu anavyojitahidi katika maisha yake yote lakini asifaulu na anapofaulu anafariki asivune bidii yake. Au mtu anafanikiwa, mfano utajiri lakini anakosa raha maisha yake yote. Kwa hivyo maisha ya mwanadamu hayaeleweki. Makala hii inanuia kubainisha sifa za wahusika wakuu katika riwaya *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili* na yale wahusika hawa walipitia katika maisha yao.

**Riwaya Rosa Mistika**

Riwaya ya *Rosa Mistika* ni riwaya ya kwanza ya Euphrase Kezilahabi iliyochapishwa mwaka wa 1971. Riwaya hii inahusu msichana mzaliwa wa kijiji cha Ukerewe aliyeitwa Rosa Mistika. Riwaya hii inaelezea maisha ya mhusika mkuu Rosa Mistika kutoka utotoni hadi kifo chake. Rosa Mistika analelewa kijiji cha Ukerewe chini ya ulinzi mkali wa babake Bwana Zakaria. Baadaye anajiunga na shule ya Misheni ya Rosary iliyosimamiwa na watawa. Katika shule ya Rosary, maisha ya Rosa mwanzoni yalikuwa ya kufurahisha kwani ndiye aliyekuwa kielelezo katika shule hiyo. Rosa Mistika alikegeuka na kupotoka kimaadili hadi akafukuzwa shuleni na baadaye anarudi kufanya mtihani. Rosa Mistika anajiunga na Chuo cha Ualimu cha Morogoro. Chuo hiki kilikuwa katika mji wa Morogoro (Tanzania) ambapo Rosa anakumbana na ukatili wa maisha ya kisasa. Vituko vya Rosa katika chuo hiki vilikuwa vingi. Rosa anashindwa kustahimili vishindo vya maisha kwa kuwa alikuwa amelelewa maisha ya kudhibitiwa na babake. Uhuru huu ulimfanya Rosa Mistika kuingilia maisha ya anasa na starehe na hatimaye kukata tama na kujiua.

**Riwaya Maisha Kitendawili**

Riwaya ya *Maisha Kitendawili* ni riwaya ya pili ya John Habwe iliyoandikwa mwaka wa 2000. Riwaya hii inahusu msichana aliyezaliwa mashambani aliyejulikana kama Farida Omar. Wazazi wa Farida ni Bwana Omar na Bi. Kibibi. Hadithi hii inaeleza maisha ya Farida kutoka mashambani hadi mjini. Farida analelewa mashambani na kupata mawaidha kutoka kwa wazazi wake. Farida alilelewa katika misingi ya kijijini na utamaduni wa kwao pamoja na mawaidha ya dini ya Kiislamu. Farida anapohamia mjini wakati anajiunga na Chuo Kikuu cha Mzalendo anakegeuka. Msichana aliyelelewa kijijini anabadilika na kuishi maisha ya mjini. Maadili yake yanabadilika na kuiga matendo ya anasa. Farida anawachezea wavulana kama Kim, Juma, Julius na wengine. Vitendo vya ukahaba alivifanya akiwa chuoni. Farida hatimaye anafuzu na shahada ya ukapera ya Arts. Baada ya maisha ya chuoni Farida alitaka aishi maisha ya ulimwengu wake bila kutegemea mtu yeyote. Hata hivyo ulimwengu ukawa karata na Farida kukosa kazi. Jambo hili lilisababisha Farida kutegemea marafiki wake ambao walisoma pamoja kama Angela na Rose. Maisha katika nyumba ya Angela na Rose yalikuwa magumu na Farida alivumilia kwa kuwa hakuwa na lingine la kufanya. Baada ya Farida kupitia changamoto nyingi za maisha kama kukosa kazi, kuteswa na marafiki alioishi nao, hatimaye alifanikiwa kimaisha. Farida anachukuwa mkopo kutoka kwa kampuni ya Juma na kuanzisha kiwanda chake cha uchapishaji. Pia Farida anaolewa na Juma aliyemdharau na kumwita mende wakiwa chuoni. Maisha ya Farida yanabadilika na kuishi maisha mema pamoja na familia yake.

**Dhana ya Wahusika**

Wahusika katika kazi ya fasihi wameelezwa na wataalamu mbalimbali. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1998) inaeleza kuwa wahusika ni watu, miti au viumbe vinavyowakilisha watu katika kazi ya fasihi. Wahusika hawa hutumiwa kuwakilisha hali halisi ya maisha ya watu katika jamii inayohusika. Senkoro (1987) anasema wahusika ni watu, ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe tabia za watu katika kazi za fasihi. Naye Msokile (1992) anaeleza kwamba wahusika husawiriwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii. Wahusika hao huelezwa kwa kutumia sifa walizonazo, jinsi walivyo, mambo yepi wanapenda na yale ambayo hawayapendi. Pia wahusika katika kazi za fasihi huwa na tabia zinazotofautiana au zinazolingana kulingana na lengo la mwandishi. Kulingana naWamitila (2008) wahusika ni nyenzo kuu katika fasihi kwa sababu wao ndio dira ya matukio na matendo yanayopatikana katika kazi ya fasihi. Kwa hivyo, wahusika huwa watendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana katika ulimwengu wa mwandishi. Naye Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza wahusika kuwa ni viumbe ambao hubuniwa kutokana na mazingira ya mwandishi. Mazingira hayo yanaweza kuwa ya kihistoria, kijiografia, kisiasa, kitamaduni na kijamii. Wahusika hawa hujadiliwa jinsi wanavyoingiliana kitabia na matendo yao. Wahusika wa aina yoyote wawe watu au viumbe hurejelea na kuakisi sifa na tabia za binadamu katika jamii husika.
Wahusika wanaweza kuainishwa kulingana na majukumu yao katika kazi ya fasihi. Wamitila (2002) anasema kuna wahusika ambao huchukuwa nafasi kuu katika kazi ya fasihi kuanzia mwanzo hadi mwisho. Hawa huwa ni wahusika wakuu. Husheheni katika hadithi nzima, matendo na migogoro ya hadithi nzima huwahusu. Kwa hivyo, makala yatadhihirisha mfanano wa wahusika wakuu katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili.*

**Wahusika walivyosawiriwa**

Katika riwaya teule za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili* wahusika wakuu ni Rosa na Farida mtawalia. Wahusika hawa wamedhihirika kuwa na sifa mbalimbali:

**Rosa Mistika**

Rosa Mistika ndiye mhusika mkuu katika riwaya ya *Rosa Mistika* kwa kuwa anatawala riwaya hii kutoka mwanzo hadi mwisho. Rosa Mistika ndiye kifungua mimba katika familia yao ya wasichana watano. Wazazi wake walikuwa Bwana Zakaria na Bi. Regina. Rosa alikuwa msichana aliyependa masomo na mwenye bidii. Tunaelezwa kuwa baada ya kufanya mtihani wa shule ya msingi Rosa anapata barua ya ushindi kutoka shule ya sekondari ya Rosary.

> Baada ya muda wa siku chache alipata barua kutoka Rosary
> ikimjulisha juu ya ushindi wake na kuchanguliwa kwake…(uk. 9).

Kutokana na bidii yake katika shule ya msingi aliweza kujiunga na shule ya upili ya wasichana ya Rosary. Pia baada ya kujiunga na shule ya upili ya Rosary aliendelea kuonyesha bidii katika masomo. Mwandishi anaeleza:

> Kweli alikuwa msichana mwenye bidii, kwani kipindi kilipokwisha
> alikuwa wa pili katika mtihani. Hivyo ndivyo Rosa alivyomaliza kipindi
> chake cha kwanza. Hivyo ndivyo alivyoweza kujitunza..(uk.22).

Walipofanya mtihani wa darasa la kumi na mbili, Rosa alidhihirisha kuwa alikuwa mwenye bidii licha ya kufukuzwa shuleni:

> Rosa alijikuta ameshinda masomo matatu, Swahili, Needle Work na English. Rosa alifurahi kuona amewazidi wengine waliokuwa pale shuleni muda wote wa masomo. Rosa alichaguliwa kwenda Morogoro TTC.Alifurahi. Zakaria na Regina walifurahi pamoja naye.. (uk. 37).

Rosa alikuwa mkware. Mhusika Rosa alifanya ngono sana hususan na watu tofauti tofauti. Rosa alikuwa kama chumba cha majaribio pale Chuo cha Ualimu cha Morogoro. Alifanya mapenzi kiholelaholela. Mwandishi anaeleza:

> Rosa alijulikana kwa kila mvulana. Alipokuwa akitoka katika chumba cha mvulana, kila mara nguo nyeupe ya ndani ilionekana chini ya gauni, na yeye mwenye akijitazamatazama (uk. 45).

Zaidi ya hayo, Rosa akiwa Chuo cha Ualimu cha Morogoro alibandikwa jina "laboratory" Jambo hili lilimaanisha kuwa Rosa alitumiwa kama nyumba ya majaribio na yeyote aliyetaka kujaribu kufanya mapenzi. Rosa alipopona aliendelea na mchezo wake. Wavulana walimzungumzia kwa vikundi wakisema:

> "Staili hii bado sijatumia, kwa nini bwana usiende lab. Lab kwenyewe ni wapi?" (uk.45).

Rosa pia anafanya mapenzi na Bwana Thomas aliyekuwa Mkuu wa Chuo. Rosa anamtembelea Bwana Thomas nyumbani kwake majira ya usiku. Mke wa mwalimu mkuu alikuwa amesafiri. Mwandishi anaeleza kuwa:

> "Rosa alimkumbatia Thomas.Thomas alikusanywa. Alivutwa, aligusa mwili wa Rosa. Wakati huo Thomas alikuwa hafahamu yuko wapi? Alikuwa amekwisha kazi. Alisema maneno mengi ( uk. 53)."

Jambo hili linadhihirisha kuwa Rosa alikuwa mkware kwa kuwa anafanya mapenzi na mkuu wa chuo baada ya kukutana naye mara ya kwanza. Pia Rosa alifahamu vyema kwamba bwana Thomas alikuwa na mke wake wa ndoa.

Rosa alikuwa mlevi. Mhusika Rosa alipenda sana kunywa pombe. Hili linadhihirika katika sehemu zifuatazo. Katika mji wa Mwanza Rosa anaamua kwenda kujifurahisha kidogo ili asahau msiba alioupata kuhusu habari za mpenziwe Deogratias kuwa na wapenzi wengi. Mwandishi anaeleza:
Rosa aliingia bar moja iitwayo " Green Bar". Humo ndani aliona mengi.

Rosa alipata meza yake peke yake pembeni na kunywa chupa yake ya Kilimanjaro kwa raha. Kijana mmoja alikuja na kukaa meza moja na Rosa. "Unatumia nini dada yangu?" Tusker, Rosa alijibu bila kuchelewa..(uk.43)

Halikadhilika, Rosa anapomtembelea Bwana Thomas nyumbani kwake wanalewa pamoja. Hili linadhihirika kupitia dondoo hii:

> Rosa alipofika alikuta Mwalimu Mkuu amemngojea kwa hamu sana. Rosa alikalia kochi moja na kabla hajasema zaidi aliulizwa " Unatumia nini, Martini au VAT 69? " Martini" Rosa alijibu akijipulizia upepo kwa kitambaa..(uk.51).

Rosa pia anakunywa pombe akiwa na Charles na dadake Flora. Huu ni wakati Rosa anachumbiana na Charles. Wakati huu Rosa alikuwa amehamia kwa mchumba wake Charles na alikuwa amemwarifu dada yake Flora kupitia kwa barua. Siku ya Flora kuja kuwatembelea anapokelewa na Charles naye Rosa alikuwa anatayarisha chakula. Baada ya kupata chakula wanaanza kunywa pombe. Mwandishi anasema:

> " Charles alileta chupa moja ya mvinyo aina ya "Grenado" .Charles alikunywa kidogo. Flora alikunywa kiasi. Rosa alikunywa kwa pupa. Charles alileta ya pili. Hii chupa ya pili ilimalizwa karibu na Rosa peke yake. Charles alimwacha mchumba wake anywe.( uk .84)."

Vitendo hivi vya Rosa vya kulewa akiwa mjini Mwanza, akiwa na mpenziwe Deogratias, akiwa chumbani kwa Bwana Thomas na akiwa na mpenziwe Charles vinadhihirisha kuwa alipenda kunywa pombe sana. Kila mara alipokuwa anatembelea mtu au yuko kwenye matembezi alipenda kulewa.
Rosa pia alikuwa mvumilivu. Mhusika Rosa alivumilia mambo mengi ambayo aliyapitia maishani mwake. Kuchapwa na baba yake baada ya kuandikiwa barua na Charles baada ya wao kukamilisha masomo ya shule ya msingi. Bwana Zakaria anamchapa Rosa hadi anavuja damu. Mwandishi anaeleza:

> Rosa alipigwa tena na tena. Makofi yalikwenda mfululizo hata damu ikamtoka puani na mdomoni. Alilia, "Baba nihurumie, sitarudia tena, nimekoma." Rosa alinyang'anywa shuka. Chupi ilimwokoa lakini matiti yalikuwa nje. Zakaria hakujali, alichukua fimbo na kuongozana mpaka chumba cha watoto…(uk.8).

Pia Rosa anavumilia mateso aliyotendewa na wanafunzi wenzake akiwa shule ya Rosary. Vitabu vyake vinararuliwa na kutiwa maji na kuchoma nguo zake. Rosa anavumilia kutegwa na marafiki wake ambao aliamini wangemuoa, kama Deogratias, Bwana Thomas na Charles. Licha ya Rosa kupitia changamoto nyingi za maisha alivumilia ila hatimaye alikumbana na mauko.

**Farida**

Farida ndiye mhusika mkuu katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Farida alikuwa kifungua mimba katika familia ya Mzee Omar na Kibibi. Katika familia ya Bwana Omar walikuwa wamezaliwa wakiwa wawili, Farida na dadake Kasu. Farida alikuwa na sifa zifuatazo: Farida alikuwa msomi. Farida anajitahidi masomoni hadi akafika chuo kikuu. Farida alijiunga katika chuo kikuu cha Mzalendo. Elimu yake inadhihirika katika siku ya kufuzu kwa mahafali katika chuo kikuu cha Mzalendo. Mwandishi anatudokezea:

> Farida alivuta hatua hadi uwanja wa Biko Square ambako sherehe za kufuzu wanafunzi zilikuwa zikiendeshwa. Farida alifanya halahala huku akiwa amevuta joho lake na taji lake. Alipata kiti chake ambacho juu yake kuliwekwa buku lenye orodha ya majina ya wanafunzi wote. (uk.73).

Zaidi ya hayo Farida anaandaa sherehe ya kufuzu kwake katika hoteli ya kifahari iliyojulikana kama Five Star Hotel International. Hili linadhihirika pale ambapo Farida anawakiribisha wageni waliofika kwenye sherehe kwa ajili ya kufaulu kwake katika masomo.

> "Nyote ningependa kuwaeleza kuwa na wakaribisha kwa wingi wa furaha ili kusherehekea kufaulu kwangu katika masomo yangu ya

digrii katika Chuo Kikuu cha Mzalendo. ( uk. 76).

Farida alikuwa mkware. Farida alipenda anasa. Farida alifanya mapenzi na wanaume kadhaa kama Kim, Julius Manono na Mkurugenzi wa Price House. Tunaelezwa:

> "Kim alihisi yeye ndiye aliyekuwa akimiliki himaya hiyo peke yake. Wengi wa wanaume walikwisha mtupa mkono, hawaji tena kwa Farida hasa kijana mmoja aliyekuwa akisoma naye. Julius Manono ambaye alionekana imara. Huyu kijana alikuwa mbeja sana. Hata hivyo alikuwa akimchezea chezea Farida tu ili apate matilaba yake...(uk 11).

Pia Farida anafanya mapenzi na mkurugenzi wa Price House ili kupata kazi. Farida anapozungumza na mkurugenzi ofisini anakubali kushwawishiwa kufanya ngono. Mkurugenzi anamshwawishi Farida kuwa wakifanya tendo la penzi atapata kazi, gari na nyumba. Mwandishi anaelezea:

> "Farida alitua kama msafiri aliyefikia mwisho wa safari yake. Mkurugenzi akapitisha mkono wake chini ya kiti chake. Farida akayatia maisha yake mtihani. Kwa hiyo ndiyo ilikuwa raslimali yake "(uk. 113).

Vitendo hivi vya Farida kufanya mapenzi na wanaume kadhaa ni ishara ya kuwa alikuwa mkware. Hakujali chochote aliwachezea wanaume kila wakati. Jambo hili linadhibitisha kuwa Farida alikuwa amekata tamaa na kuona maisha hayana maana na kuingilia anasa bila kujali.
Farida pia alikuwa mlevi. Alipenda sana kunywa pombe kila wakati alipoenda matembezi. Mwandishi anaeleza kuwa Farida alipotembea ukumbini Kibokoni akiwa na Kim alilewa pombe aina ya Guiness hadi ulevi ukawazidi. Jambo hili lilisababisha Farida kumwacha mpenziwe Kim na kuenda nyumbani kwa Papi:

> "…Tena alisema Kim na kumwagizia mwuza baa na kumwambia, leta Guiness saba hapa na glasi mbili ... (uk. 10).

Baada ya Farida kufuzu aliandaa sherehe katika hoteli maarufu Five Star Hotel International. Marafiki wa Farida na wale waliosoma naye walihudhuria kwenye sherehe. Vyakula vya kila aina viliandaliwa pamoja na vinywaji. Mwandishi anaeleza:

> Vinywaji vilianzia kumwagwa, na wale ambao walikuwa hawajamaliza chakula walifanya haraka. Kulikuja Whisky, Red Wine, Tusker, Guiness, Martel na Kingfisher. Kila mmoja alichagua pendo lake...(uk. 78).

Farida alikuwa mvumilivu. Farida anavumilia mateso aliyopitia akiwa nyumbani kwa Angela na Rose. Farida baada ya sherehe ya kufuzu anaishi kwa Angela. Kwa kuwa Angela alikuwa amebahatika kupata kazi. Farida alimtegemea kwa kila kitu pale nyumbani. Angela alipoanza kuona Farida kama mzigo, alianza kuja nyumbani usiku sana na kulala. Angela siku moja alifika nyumbani akiwa amelewa pamoja na rafiki yake Moses Mtoro. Walifika wakipiga kelele na kugonga mlango kwa fujo bila sumile. Angela anamkaripia Farida anapofungua mlango.

> "… Mbona tunangoja karibu kuvunja mlango na wewe unastarehe tu. Huna wasiwasi? Angela alimuuliza Farida waziwazi huku

amemweka macho yake ya kilevi ..”(uk 92).

Farida anavumulia mateso hayo na kuendelea kuishi kwa Angela. Pia Farida anavumilia kuishi nyumbani kwa Rose. Farida alitegemea Rose kwa kila kitu alichohitaji pale nyumbani. Mwandishi anelezea:

> “Faridia alikuwa kama mtu wa kazi wa Rose. Mapishi ni yeye, ufuaji wa nguo ni yeye, udekaji wa sakafu ni yeye na ununuzi wa vitu vidogo vidogo ni yeye. Maskini alivumilia mradi akae siku moja zaidi.”(uk. 101)

Farida alivumilia kuishi nyumbani kwa Rose licha ya mateso aliyopitia mikononi mwa mhusika Rose. Farida alitamani kuondoka lakini swali kubwa lililomkabili ni kuwa aondoke akielekea wapi? Kwa hivyo ilimbidi kuvumilia kuishi nyumbani kwa Rose licha ya mateso aliyopitia, kwa kuwa lisilo budi hutendwa.

**Yaliyopitiwa na mhusika Rosa na Farida katika maisha yao**

**Mhusika Rosa Mistika**

Mhusika Rosa Mistika alipitia changamoto nyingi za maisha kabla hajakata tamaa. Kwanza Rosa alilelewa kijijini na kudhibitiwa na babake Zakaria. Bwana Zakaria aliamini kuwa mabinti huchungwa kama mahabusu ili wasitangamane na wavulana. Kasumba hii ilisababisha Rosa kuadhibiwa kinyama na Bwana Zakaria baada ya kuandikiwa barua na Charles.

Rosa Mistika alizaliwa katika familia maskini. Jambo hili linadhihirika pale ambapo Rosa anapata barua ya kujiunga na shule ya Rosary. Kwa kuwa familia hii haikuwa na pesa ilibidi mamake Rosa Bi. Regina kupika pombe na kusaidiwa na Rosa kuuza ili wapate karo ya shule. Rosa alipojiunga na shule ya Rosary anadhulumiwa na wanafunzi kwa kuchomewa nguo na vitabu vyake kutiwa kwenye maji. Zaidi ya hayo, baada ya Rosa kubadili tabia na kuwa anafanya kinyume na sheria za shule anafukuzwa shuleni hadi siku ya kufanya mtihani.

Katika Chuo cha Ualimu, Rosa anafanya mapenzi na mkuu wa chuo ambapo wanafumaniwa na mke wa Bwana Thomas. Jambo hili linasababisha Rosa kupata majeraha usoni mwake na kukatwa sikio. Baada ya tukio hili Rosa anafukuzwa chuoni na mwalimu mkuu Bwana Albert ila baadaye anapewa cheti cha kufuzu kuwa mwalimu.

Masaibu yanazidi kumpata Rose baada ya kukataliwa na mpenzi wake Charles. Rosa baada ya kutulia kimaisha na kuamua kuolewa na kumpata mpenzi wake Charles tena, ndoa yao inatamatika pale ambapo Charles alitambua kuwa Rosa si bikira. Jambo hili linasababisha Rosa kukata tamaa, kuona maisha hayana maana tena baada ya kukataliwa tena na Charles. Matumaini yake yalikuwa kwake baada ya kubadilisha mwenendo wake na kupata utulivu alipokutana na Charles tena. Mhusika Rosa Mistika anastahimili matatizo yaliyomsibu na kupambana na maisha na kujiona amefaulu lakini anajiua kwa kuona maisha hayana maana.

**Mhusika Farida**

Farida alipitia mengi akiwa kijijini na mjini. Kwanza Farida alizaliwa katika familia iliyokuwa fukara. Hili linadhihirika kupitia hali ambayo Farida waliishi. Familia yao haikuwa na pesa za kumpeleka baba yao hospitali. Pia kupata chakula na malazi katika familia hii ilikuwa tabu. Mfano Farida walilalia matandikio yaliyoliwa na mchwa. Wazazi wa Farida kufariki wakiwa wachanga. Bwana Omar na Bi. Kibibi wanapofariki Farida anahamia kwa mjomba wake Bwana Marufuku. Jambo hili linasababisha Farida kukosa malezi mema na upendo kwa mzazi. Baada ya Farida kuingia mjini maisha yake yanabadilika. Farida akiwa chuoni anafanya mapenzi na Kim kwa matumani ya kuwa ataolewa na yeye. Farida aliona mahusiano hayo yangeishia katika ndoa ila yote haya yaliishia kuwa kitendawili. Kifo cha Kim kinampotezea matumaini Farida kwa kuwa alikuwa ameahidiwa kazi na pia kuolewa na

Kim.

Farida baada ya kukamilisha masomo yake ya chuo, anasaka kazi bila mafanikio. Jambo hili linaonyesha Farida akiishi kama mtumwa kwa Angela na baadaye kwa Rose. Alipitia changamoto nyingi sana hadi kuona maisha hayana maana kwake. Zaidi ya hayo Farida analazimishwa kufanya mapenzi na mkurugenzi mkuu wa kampuni ili kupata kazi. Baada ya kufanya mapenzi hakupata kazi aliyokuwa ameahidiwa. Hatimaye Farida alichukuwa mkopo na kuanzisha bisashara yake na kujiendesha kimaisha. Farida anakutana na Juma, aliyekuwa mpenzi wake wakiwa chuoni na kufunga ndoa. Wanafanikiwa na mtoto kwa jina Faki. Farida alipitia chamgamoto ila hakupoteza matumaini.

**Hitimisho**

Ingawa riwaya hizi mbili ziliandikwa katika nyakati tofauti na waandishi tofauti zina mfanano wa fani hasa katika kipengele cha wahusika. Wahusika wakuu katika riwaya *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili* ni wa jinsia ya kike. Riwaya hizi zote mbili zinahusu wasichana washamba ambao ni limbukeni wa maisha. Pia wahusika wote wakuu katika riwaya teule wamezaliwa katika familia ambazo ni za tabaka la chini lililojaa umaskini na wahusika hao walilelewa kwa kudhibitiwa sana.

Uwiano zaidi unapatikana katika sifa zao zinazotambulika kutokana na vitendo vyao. Baadhi ya sifa hizo ni; wote walikuwa wanapenda kusoma kwa kuwa wote walipata vyeti mbalimbali. Walikuwa walevi, Farida na Rosa Mistika walipenda kulewa sana wanapoenda matembezi. Pia wahusika hawa wakuu walikuwa na sifa ya kuvumilia. Wote walipitia changamoto nyingi ila wakavumilia na kufanikiwa licha ya Rosa Mistika kukata tamaa.Waandishi wote walidhihirisha kuwa wahusika hawa walikuwa wakware. Farida na Rosa Mistika walipenda anasa sana na walichezea wanaume kila mara. Wote hatimaye walikutana na wapenzi wao wa awali. Rosa alikutana na Charles, wakarudiana lakini hawakuoana. Farida naye mwishowe alikutana na Juma, wakapendana tena na wakaoana.

Katika riwaya hizi mbili za Euphrase Kezilahabi na John Habwe, tumeweza kuthibitisha kuwa waandishi hawa wametilia makazo matatizo halisi yanayomsibu mwanadamu, na juhudi za mtu kupambana na maisha huishia kukegeuka au kukata tamaa. Pia matokeo ya uhakiki huu yamedhihirisha kuwa waandishi hawa wametumia wahusika wakuu wenye sifa sawia.

**Funding:** This research received no external funding.

**Acknowledgments:** I acknowledge the diverse support offered by the Ministry of Education in Machakos town sub-county.

**Conflicts of Interest:** The author declared no conflict of interest.

**Disclaimer Statement**

This article is part of my on-going M.A studies at the Department of Linguistics and Languages, Machakos University.

**Authors Bionotes**

Shadrack Tete Muia holds a Bachelor of Education Arts degree in Kiswahili and is currently pursuing Master of Arts in Kiswahili at Machakos University, Kenya. His research interests are in Kiswahili Fasihi. John Mutua teaches Kiswahili and serves as the current chair, Department of Linguistics and Languages, Machakos University. Vifo Makoti is a senior lecturer and teaches Kiswahili and translation studies at Machakos University.

**Marejeleo**

Euphrase, K. (1971). *Rosa Mistika*. Nairobi. Kenya Litrature Bureau.

Habwe, J. (2000). *Maisha Kitendawili*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar-es- Salaam University Press.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*: Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Senkoro, F. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar-es- salaam: Press and Publicity Centre.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers L.t.d.

_________(2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.

_________ (2008). *Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi. Vide Mulwa Publishers L.t.d.

Wafula, R., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*: Nairobi. Sai Industries Limited.

Wanjala, F. S. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza : Serengeti Publishers.